BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 24 Mei, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

126. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kama inavyofahamika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ni Taasisi za Muungano ambazo zinatekeleza mambo ya Muungano. Hata hivyo ajira katika Taasisi hizo hazionyeshi sura halisi ya Muungano kama vile uwepo wa asilimia 21 ya wafanyakazi kutoka Zanzibar na wajumbe wa kutosha wa bodi kutoka Zanzibar.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi kutoka Zanzibar wameajiriwa kama wafanyakazi na kuteuliwa katika bodi za TCRA na TCAA na ni asilimia ngapi ya wafanyakazi na wajumbe wa bodi wote.

(b) Je, muundo wa bodi za TCRA na TCAA unaozingatia uwakilishi wa Zanzibar umetekelezwaje ndani ya miaka 10 iliyopita.

(c) Je, katika gawio la asilimia 4.5 inayotakiwa kupatiwa Zanzibar, TCRA na TCAA imezipatia kiasi gani, katika akaunti ipi na kwa utaratibu upi katika miaka 10 iliyopita.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi wa Uwekezaji:</u>**

129. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kumekuwa na taarifa mbali mbali za Serikali za kuvikodisha visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar. Hata hivyo, kunaonyesha kuwepo kwa ushirikishwaji mdogo wa wadau na wananchi husika wa Zanzibar hasa katika hatua za awali na za kutoa maamuzi. Mfano mzuri ni wa kisiwa kidogo cha Matumbini ambapo hadi sasa hatma ya wananchi wake haijuilikani.

(a) Je, ni upi utaratibu wa kuvitia bei visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar kabla ya kuvikodisha.

(b) Je, visiwa vilivyokodishwa au kukusudiwa kukodishwa, vimekodishwa au vitakodishwa kwa bei gani na kwa muda gani.

(c) Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha shughuli za wananchi wakiwemo wavuvi wanaoenda dago haziathiriki.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la hatari ya wanafunzi kupata ajali kutokana na vyombo mbali mbali katika maeneo ya vivuko wakati wa kwenda na kurudi skuli.

(a) Je, Wizara yako inalitambua hilo.

(b) Je, Wizara ipo tayari kuweka usimamizi imara pamoja na kuhuisha alama za barabarani katika maeneo kama vile Taveta, Nyumba mbili, Mwanakwerekwe C, na eneo la kivuko cha skuli ya Nyerere.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

147. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Inafahamika kwamba, sio lengo la Serikali kuwabagua wananchi wake katika kupata huduma za msingi ikiwemo huduma ya elimu bora. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuhusu upatikanaji wa huduma ya elimu katika baadhi ya vijiji ndani ya jimbo la Pandani. Kwa mfano, katika kijiji cha Mvimbe kuna vyumba viwili tu vya maandalizi kwa wanafunzi zaidi ya 80 wa kuanzia.

(a) Je, Serikali inavitambua vyumba hivi viwili vya maandalizi katika kijiji cha Mvimbe.

(b) Je, ni lini Serikali itajenga skuli rasmi ya maandalizi katika kijiji cha Mvimbe.

(c) Je, ni lini Serikali itaanza kuipatia skuli ya maandalizi ya Mvimbe walimu na vifaa vya kutosha vya kusomea.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

128. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Itakumbukwa kwamba Serikali iliridhia kuwepo kwa Mradi wa Kufuga Samaki utakaoendeshwa kwa mashirikiano na Kampuni kutoka nchi za Norway na Oman ambapo sehemu ya mpango huo ilielezwa katika Baraza la Wawakilishi na katika Mkutano wa Bajeti. Hata hivyo, kumekuwa na kusuasua kwa maendeleo ya mradi huo kiutekelezaji.

(a) Je, ni maeneo gani ya Unguja na Pemba yatakuwa yamehusishwa na Mradi huu hadi kukamilika kwake.

(b) Je, mradi huo ni wa miaka mingapi na gharama gani na umefikia wapi kiutekelezaji.

(c) Je, Serikali ina mchango gani na inatarajia kupata faida

gani kutoka katika mradi huo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

148. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kuwapatia wakulima wetu vifaa maalum vya kupima udongo ili kuondokana na kilimo cha mazoea.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**24 Mei, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**